JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI
(OSHA)

TAARIFA YA MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI YA MWAKA 2003

DAR ES SALAAM **21 OKTOBA, 2021**

Yaliyomo

1. UTANGULIZI 1
1.1. Dira 1
1.2. Dhima 1
1.3. Majukumu ya Wakala 1
1.4. Kazi za Wakala 2
1.5. Ofisi za Wakala 2
1.5.1. Ofisi za Mikoa 2
2 . TAARIFA YA MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI YA MWAKA 2003. 3
3. HITIMISHO 9

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Occupational Safety and Health Authority) –OSHA unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi Namba 5 ya Mwaka 2003. Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kusimamia Afya na usalama mahali pa kazi.

1.1. Dira

Kuhakikisha sehemu za kazi zinazingatia Usalama na Afya.

1.2. Dhima

Kusimamia, Kuelimisha na Kuhamasisha masuala ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa kuweka mifumo thabiti itakayo zuia ajali, magonjwa, na vifo pamoja na uharibifu wa mali ili kupunguza gharama za uendeshaji na kukuza uchumi wa Taifa.

1.3. Majukumu ya Wakala

Mheshimiwa Mwenyekiti, OSHA ina majukumu Makuu yafutayo: -

a) Kusimamia Utekelezaji wa Sheria Namba 5 ya Mwaka 2003 ya Usalama na Afya na Mahali pa Kazi na Kanuni zake ili kuhakikisha wafanyakazi wanatekeleza majukumu yao katika mazingira ya usalama na afya; kwa kufanya Kaguzi za usalama na afya kwenye maeneo ya kazi;

b) Kuishauri Serikali kuhusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi, kuhusiana na Sera, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya usimamizi wa usalama na afya nchini ikiwemo kushauri namna ya kuridhia mikataba ya kimataifa inayohusu masuala ya usalama na afya;

c) Kuongeza uelewa wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi kwa kutoa mafunzo ya usalama na afya kwa waajiri na wafanyakazi ikiwemo ushauri wa kitaalamu; na

d) Kufanya tafiti zinazohusiana na masuala ya usalama na afya sehemu za kazi ili kuweza kuishauri Serikali namna bora ya kutekeleza Sheria tajwa.

1.4. Kazi za Wakala

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Sheria Namba 5 ya Mwaka 2003, Wakala unatekeleza kazi zifuatazo;

a) Kusajili sehemu za kazi;
b) Kufanya Ukaguzi wa Jumla (General Inspections);
c) Kufanya Ukaguzi Maalum kama, Ukaguzi wa Usalama wa Umeme, Vyombo vya Kanieneo (Pressure Vessels), na Ukaguzi wa vifaa vya kunyanyulia vitu vizito (Lifting Appliances);
d) Kutathmini hatari zilizopo mahali pa kazi (Risk Assessment);
e) Kufanya Uchunguzi na uidhinishaji wa michoro na ramani;
f) Kufanya Uchunguzi wa Afya na magonjwa kulingana na kazi husika mahali pa kazi;
g) Kufanya Uchunguzi wa ajali (Accident Investigation);
h) Kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira ;(Occupational Hygiene Surveys and Measurements) na
i) Kufanya tathmini za Kiegonomia.

1.5. Ofisi za Wakala

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kusogeza huduma kwa wananchi Wakala una Ofisi katika Kanda sita (6) na Mikoa mitano (5) kama ifuatavyo:

a) Kanda ya Pwani (inajumuisha Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro) yenye makao makuu mkoani **Dar es Salaam**;
b) Kanda ya Ziwa (inajumuisha Mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Shinyanga, Simiyu, na Geita) yenye makao makuu mkoani **Mwanza**;
c) Kanda ya Kati (inajumuisha mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma) yenye makao makuu **jijini Dodoma**;
d) Kanda ya Kusini (inajumisha Mikoa ya Lindi, Mtwara, na Ruvuma) yenye makao makuu Mkoani **Mtwara**;
e) Kanda ya Nyanda za juu Kusini (inajumuisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Songwe, Katavi, Rukwa, Njombe) yenye makao makuu mkoani **Mbeya** na
f) Kanda ya Kaskazini (Mikoa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Manyara) yenye makao makuu mkoani **Arusha**.

1.5.1.Ofisi za Mikoa

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wakala una ofisi katika Mikoa ya Morogoro, Njombe, Tanga, Shinyanga na Tabora. Aidha, OSHA inatarajia kufungua Kanda mpya ya Magharibi, itakayojumisha Mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi.

2. TAARIFA YA MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI YA MWAKA 2003.

2.1. MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA SHERIA

2.1.1. Kuiwezesha Tanzania kutambulika katika Nchi za SADC katika masuala ya Usalama na Afya mahali pa Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita OSHA imeiwezesha Tanzania kupata **Dawati la Usalama na Afya mahali pa Kazi** katika Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nafasi hii muhimu kwa Nchi yetu kuweza kuuza na kubadilishana Utaalamu wa Mifumo ya Uendeshaji wa Taasisi za Usalama na Afya Kimataifa ilishindanisha **wataalamu 48 kutoka katika Nchi 16** katika Jumuiya ya SADC na Tanzania kupitia OSHA, iliibuka mshindi wa nafasi hiyo **kutokana na kuwepo kwa mfumo madhubuti ya Usalama na Afya mahali pa kazi; usimamizi bora wa nguvu kazi na uwepo wa ajira zenye staha**.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hatua hii ni Mafanikio makubwa kwa nchi yetu na OSHA kwa kutambulika Kimataifa kwa kuwa na wataalam wenye uwezo wa kusimamia mfumo ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa kuzingatia vigezo vya Kimataifa ambapo mwakilishi huyo mkazi atakuwa **nchini Botswana** ili kushauri namna bora ya kuwezesha masuala ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi katika Nchi za SADC.

2.1.2. Kuondoa Ada na Tozo mbalimbali

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utafiti uliofanywa na Wakala kuhusu usajili wa sehemu za kazi pamoja na kushughulikia malalamiko ya Wawekezaji na wafanyabiashara OSHA ilibaini kuwepo kwa tozo ambazo zilikuwa zikilalamikiwa kuwa zinaongeza gharama za uendeshaji na kuchangia sehemu nyingi za kazi kutojisajili na kufanya ushindani wao kibiashara kuwa mgumu, na hivyo OSHA ilipendekeza tozo hizo kufutwa. Serikali iliridhia hoja hiyo kwa kufanya marekebisho kupitia GN 719 ya tarehe 16 Novemba **2018**, GN 999 ya tarehe 13 Novemba **2020** na **GN 496F ya Tarehe 30 Juni 2021** kwa kuondoa **tozo 11** kama ifuatavyo: -

a) Kuondoa Ada ya Usajili wa eneo la kazi iliyokuwa ikitozwa kati ya Sh. 50,000/= hadi Sh.1, 800,000/=;
b) Kuondoa Ada ya fomu ya usajili sehemu za kazi iliyokuwa ikitozwa Sh. 2,000/=;
c) Kufuta Faini zinazohusiana na vifaa vya kuzimia moto ya Sh. 500,000/=;
d) Kuondoa Ada ya Leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi iliyokuwa inatozwa Sh. 200,000/= kwa mwaka;
e) Kuondoa Tozo ya Ushauri wa kitaalamu wa Usalama na Afya ya Sh. 450,000/= kwa saa kwa mtaalam.
f) Kufuta tozo ya mafunzo ya elimu kwa umma iliyokuwa inatozwa kiasi cha sh. 250,000/= kwa kila mshiriki;
g) Kupunguza ada ya uchunguzi wa ajali iliyokuwa ikitozwa sh. 500,000/= kwa kila mtaalam anayefanya uchunguzi hadi sh. 120,000/= kwa kila mtaalam lakini si zaidi ya sh. 1,000,000/= na
h) Kupunguza Ada na Tozo nne za Umeme katika Vituo vya Mafuta Vijijini za;
    i) **Umeme ya *Polarity test per point*** katika vituo vya mafuta vilivyopo katika maeneo ya vijijini;
    ii) **Umeme ya *Continuity Test per point*** katika vituo vya mafuta vilivyopo katika maeneo ya vijijini ;

iii) **Umeme ya *Earth Resistance Test* point** katika vituo vya mafuta vilivyopo katika maeneo ya vijijini na

iv) **Umeme ya *Insulation Test per point*** katika vituo vya mafuta vilivyopo katika maeneo ya vijijini.

Hivyo kufanya tozo za umeme katika vituo vya mafuta vijijini kupungua kutoka Sh. 650,000/= hadi Sh. 150,000/=. Punguzo hili linatarajiwa kuvutia uwekezaji zaidi katika maeneo ya vijijini na hivyo kupunguza athari ya utunzaji wa mafuta kwenye chupa za maji na madumu, suala ambalo linahatarisha maisha ya wananchi katika maeneo hayo.

Tozo zilizofutwa zimeweza kuleta unafuu kwa Wafanyabiashara na Wawekezaji Nchini kwa kuwapunguzia gharama za uendeshaji kwa kiasi cha **zaidi ya Sh. Bilioni 35 endapo zingeendelea kutozwa.**

2.1.3.Kupunguza Urasimu na Uboreshaji wa Mifumo ya TEHEMA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala umeendelea na Mapitio ya Mlolongo wa shughuli (Business Process Review) ili kupunguza urasimu katika utoaji huduma, ambapo OSHA imeweza kuondoa urasimu katika utoaji wa vyeti na leseni za kukidhi viwango vya usalama na Afya kwa kufanya yafuatayo: -

a) Kupunguza muda wa kupata Cheti cha Usajili wa sehemu za kazi (Registration Certificate) **kutoka siku 14 hadi siku 1 kwa sasa na kwa njia ya kieletroniki na ambapo mteja ana uwezo kuprinti cheti chake cha usajili popote alipo (Online registration).**

b) Kupunguza muda wa kutoa leseni ya Kukidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya mahali pa kazi (Compliance License) kutoka **siku 28 hadi siku 3 kwa sasa**; na

c) Kusimika mfumo wa TEHAMA wa Usimamizi wa taarifa za kaguzi nchini (Workplace Inspection Management System - WIMS) ambapo kupitia mfumo huu, huduma ya utoaji wa taarifa za ukaguzi, ajali na mafunzo unafanyika kwa njia ya kieletroniki hivyo kusogeza huduma zaidi.

Aidha, Mfumo wa WIMS unawapa uwezo waajiri **kusajili maeneo ya kazi, kuomba mafunzo, kutoa taarifa za ajali, kuwasilisha nyaraka na kujifanyia tathmini ya hali ya usalama na afya** wakiwa katika maeneo yao ya kazi. Kupitia mfumo huu, Waajiri wanaweza kujifanyia tathmini ya namna **walivyokidhi viwango vya usalama na afya (Self-Assessment)** na hivyo kurahisisha upatikanaji wa leseni ya kukidhi viwango vya usalama na afya.

2.1.4.Kuanzisha *MEDIA HOUSE* ya Usalama na Afya

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto ya uelewa mdogo wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi OSHA imeanzisha *Media House* yake kwa ajili ya;-

a) Uzalishaji wa Vipindi vya Elimu kwa Umma kinachoitwa Kazi **"Kazi Salama, Maisha Salama**" ambapo katika kipindi cha Mwezi Mei 2021 hadi Septemba 2021 jumla ya vipindi 26 vilirushwa hewani kwa ajili ya kutoa elimu ya Usalama na afya katika sekta za Madini, Kilimo na Sekta ya Ujenzi ikiwa ni pamoja na Wajasiriamali wadogo nchini vipindi hivyo vilirushwa kupitia TBC, Channel Ten, ITV, Azam TV, Wasafi TV, Clouds TV na Star TV;
b) Usimamizi na Uwekaji wa taarifa (Content) katika mitandao ya kijamii katika akaunti za OSHA katika mitandao ya Instagram (osha_tanzania_official), Twitter (@Tanzaniaosha) na Facebook (OSHA Tanzania) na
c) Usimamizi wa **TV Channel** ya OSHA kupitia Mtandao wa **Youtube (OSHA TV Online)** pamoja na uingizaji wa vipindi kwa ajili ya kuelimishwa umma.

2.1.5. Uratibu wa Ukaguzi wa Kisekta (Sectorial Inspections)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala unatekeleza Mkakati mwingine wa kuhamasisha Wawekezaji walio na matawi mengi katika mikoa mbalimbali nchini kuratibu shughuli za Ukaguzi, Mafunzo na Upimaji Afya kupitia ofisi zao za makao makuu ili: -

a) Kuwezesha sehemu za kazi kupanga ratiba ya kaguzi na masuala ya kibajeti yanayohusu Usalama na Afya;
b) Ziweze kufanyiwa kaguzi, Mafunzo na upimaji Afya kwa wakati mmoja badala ya kila ofisi moja moja kufanya ukaguzi kwa wakati wake;
c) Kurahisisha upatikanaji wa Leseni ya kukidhi matakwa ya Usalama Mahali pa kazi kwa kutolewa kwa ofisi na matawi yote ya sehemu za kazi nchini; na
d) Kuwezesha Menejimenti kupata mrejesho wa Jumla wa hali ya Usalama na Afya katika maeneo yao yote nchini kwa wakati.

2.1.6. Kuimarisha Ushirikiano na Wadau

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulitekeleza hili OSHA inafanya yafuatayo: -

a) OSHA inashirikiana na Taasisi nyingine za Kiserikali Kama Vile Shirika na Viwango la Taifa (TBS) katika kutengeneza viwango vya usalama na afya nchini (OSH Standards), Mkemia Mkuu wa Serikali katika kubadilishana taarifa, ERB, REA na CRB katika kutambua miradi mbalimbali inayoanzishwa nchini pamoja na NBS, BRELA, TRA katika kupata taarifa

za maeneo ya Kazi nchini, NIDA katika kupata taarifa za Wafanyakazi, Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (TIC) kwa kuimarisha dawati la pamoja kufanya usajili wa papo kwa hapo,

b) Kuimarisha ushiriki katika programu mbalimbali zinazoendeshwa na Wizara ya Viwanda na Biashara hasa katika kuboresha Mazingira ya Kufanyia biashara nchini kupitia Business ***clinic***, na

c) Wakala umekuwa ukifanya ukaguzi wa pamoja pale inapobidi na taasisi za Serikali kama vile Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Idara ya Kazi, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ili kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi nchini.

2.1.7. Programu Atamizi ya Wajasiriamali (SMEs Incubation Programme)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala umefikia sekta isiyo rasmi hasa wakinamama wasindikaji na Wenye Viwanda Vidogo chini ya SIDO, Vikundi vya Wenye Ulemavu pamoja na wachimbaji wadogo wa migodi nchini kupitia mashirikiano mbalimbali kwa kuzindua **Programu Atamizi ya Wajasiriamali** nchini yenye kauli mbiu ya **"Afya yangu Mtaji Wangu"** ambayo inajumuisha yafuatayo: -

a) Kutekeleza programu ya mafunzo bure kwa Wajasiriamali Wadogo ambapo kwa Mwaka wa fedha wa 2020/21 jumla ya Wajasiriamali **9,630** wamepewa mafunzo ya usalama na Afya mahali pa kazi;

b) Kutoa vifaa kinga kwa Wajasiriamali wadogo ili waweze kujikinga na athari za kiusalama na afya mahali pa kazi na

c) Kuzindua **mfumo wa Kieletroniki (SMEs Online registration) uliowawezesha Wajasiriamali 369 kujisajili** na kufikiwa katika maeneo yao na kuelimishwa pamoja na kushauriwa namna bora ya kuboresha mazingira yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupitia programu hii Wajasiriamali wanatambuliwa na kulelewa, kuelimishwa, kukaguliwa na kuwawezesha kujirasimisha ambapo OSHA imeandalaa mwongozo mahususi wa Mafunzo ya Usalama na Afya pamoja na Viwango stahiki (OSH Standanrds) vya kukidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya ili kuwaongezea ushindani wa kibiashara na masoko ya bidhaa zao.

2.1.8. Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kupunguza ajali, magonjwa na vifo vinavyotokana na mazingira ya Kazi, Wakala hufanya kaguzi za Usalama na Afya mahali pa Kazi. Kaguzi hizo zinajumuisha kaguzi wa Usalama wa Umeme, Mitambo ya kuzalishia mvuke (Boilers), Mitungi ya gesi na hewa (Air receivers), Majengo na Majenzi, Egonomia, Zana za kunyanyulia vitu vizito, Vipimo vya Ubora wa mazingira ya Kazi pamoja na Upimaji Afya za Wafanyakazi nchini vikiendana na utoaji wa mafunzo ya Usalama na Afya mahali pa Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala uwemeza kuongeza idadi ya kaguzi zinazofanyika kwa mwaka kutoka kaguzi 85,491 katika Mwaka wa fedha wa 2016/2017 hadi kufikia Kaguzi **193,385** kwa Mwaka wa fedha wa **2020/2021** ambapo kumekuwa na ongezeko la upimaji afya kutoka Wafanyakazi 61,613 kwa Mwaka hadi kufikia Wafanyakazi **283,348** kwa Mwaka. Halikadhalika, kumekuwa na ongezeko la Wafanyakazi wanaoelimishwa kuhusu masuala ya Usalama na afya Kutoka Wafanyakazi 4,093 kwa Mwaka wa fedha wa 2016/2017 hadi kufikia Wafanyakazi **9,172** katika Mwaka wa fedha wa 2020/2021 kama inavyoonekana katika mchoro hapa chini;



Chanzo (Taarifa za OSHA)

2.2. CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA SHERIA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi umeendelea kuendesha shughuli zake kulingana na bajeti iliyopitishwa na kwa kuzingatia Sheria, Taratibu, Miongozo na mifumo iliyopo ya Usimamizi. Aidha, katika kutekeleza majukumu yake kumekuwa na masuala ambayo yalihitaji kufanyiwa maboresho. Masuala hayo ni kama yalivyoainishwa katika jedwali hapa chini;

Na	ENEO LA MABORESHO	MIKAKATI
1.	Uhaba wa Watumishi	a) Wakala unaendelea kuongeza idadi ya Wafanyakazi wa Usalama na Afya ambapo katika ikama ya Mwaka wa

Na	ENEO LA MABORESHO	MIKAKATI
		fedha wa 2021/22 **vibali vya kuajiri Wafanyakazi wapya 136** vinashughulikiwa ili kuongeza nguvu kazi; b) Sambamba na hili Wakala umeanza kufanya majadiliano ya ndani na Taasisi nyingine za Kiserikali ili kuweza kupata wataalamu (Head hunting) hivyo kupunguza uhaba wa wafanyakazi; na c) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA ambapo kutapunguza uhaba wa Watumishi kwa kiwango kikubwa hasa kwa kuanzisha mifumo ya kieletroniki itakayorahishisha mlolongo wa shughuli (Business Process).
2.	Ongezeko la Vihatarishi vya Usalama na Afya linalochangiwa na mabadiliko ya teknolojia za Kisasa.	Wakala unaendeleza Mikakati ya kuwaongezea Ujuzi Wakaguzi wa Usalama na Afya mahali pa kazi pamoja na Kuendelea kuwapatia vifaa vya kisasa vinavyoendana na mabadiliko ya teknolojia ili kuweza kushauri ipasavyo maeneo ya kazi. Sambamba na hilo Wakala umeanza kutumia *Drones* katika ukaguzi wake ili kufikia maeneo hatarishi zaidi na Kupunguza athari za kiusalama kwa Wakaguzi.
3.	Uelewa mdogo wa masuala ya Usalama na Afya miongoni mwa wadau.	Wakala umeweka mikakati ya kuendesha semina, mikutano na makongamano na wadau wa kila sekta ukijumuisha wajasiriamali wadogo. Aidha, Wakala unashiriki matukio mbalimbali ya kitaifa kama vile Sabasaba, Nanenane, Maadhimisho ya Mwenge, Siku ya Vijana, na kutoa tuzo kwa washiriki wa maadhimisho ya siku Afya na Usalama Duniani kila Mwaka ili kuleta mwamko wa masuala ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi.

3. HITIMISHO

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), kwa heshima na taadhima unawasilisha taarifa ya Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi; Kwa kutekeleza Mikakati hiyo, kumekuwa na ongezeko la sehemu za kazi hadi kufikia sehemu **26,740** zilizosajiliwa kwa Mwaka 2020 ikilinganishwa na sehemu za kazi **11,963** zilizosajiliwa Mwaka 2018. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 223** na inaashiria kuwa, maeneo mengi ya kazi yamefikiwa na kukaguliwa, Wafanyakazi wengi

wamepimwa afya zao, kwa mantiki hiyo hali ya usalama na afya maeneo ya kazi inazidi kuimarika. Aidha, Wakala unaendelea kubuni na kutekeleza Mikakati mbalimbali ya kulinda usalama wa Wafanyakazi katika kuimarisha Uchumi wa Viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima ninaomba kuwasilisha.

Mhe. Jenista J. Mhagama (Mb)
WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU.